BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 31 Mei, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI YA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2018/2019.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Mwaka 2018/2019.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

110. MHESHIMIWA HIDAYA ALI MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tangu utekelezaji wa Sera ya ugatuzi uanze kumekuwa na changamoto kadhaa za utekelezaji moja wapo ikiwa baadhi ya shughuli zilizogatuliwa hasa kwenye sekta ya kilimo hazijakabidhiwa rasmi kwa Serikali za Mitaa ili waweze kuzitekeleza kwa ufanisi.

Je, kuna sababu gani inayopelekea majukumu hayo kuchelewa kukabidhiwa rasmi kwa Serikali za Mitaa.

Wizara ya Fedha na Mipango:

124. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Serikali katika kuleta maendeleo ya wananchi wake, imetoa fursa ya uanzishaji wa mabenki ili kutoa mikopo kwa wananchi kwa lengo la kujiendeleza kimaisha. Hata hivyo, riba zinazotozwa na benki hizo ikiwemo Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni kubwa sana.

(a) Je, Serikali inalionaje suala hili la riba kuwa kubwa na kupunguza.

(b) Je, kwa mabenki ya binafsi kuna utaratibu wa Sheria wa kuwapangia kupunguza viwango vya riba.

(c) Je, kama mabenki ya binafsi hayataki kupunguza riba, Je benki yetu ya PBZ inalionaje suala hili la kupunguza riba.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

135. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na utaratibu wa kuweka namba mpya za gari za abiria hasa zinazokwenda mashamba. Utaratibu wa zamani namba zinafuatana mfano namba 1 Mkokotoni, namba 2 Bumbwini, namba 3 Mndo, namba 4 Pwani Mchangani, namba 5 Ndagaa, namba 6 Chwaka, namba 7 Bweleo, namba 8 Unguja Ukuu, namba 9 Bwejuu, namba 10 Makunduchi, namba 11Binguni.

(a) Je, kwanini utaratibu huu mwepesi wa kuweka namba za gari umeondoshwa na badala yake umekuja utaratibu mpya wa namba mpya na majina.

(b) Je, kwanini utaratibu huu mpya wa kuweka majina ya maeneo hayo usibakishe nambari za asili kama zilivyokuwa zikifuatana na majina.

(c) Je, wahusika katika sekta ya usafirishaji abiria nchi kavu wanashirikishwa katika mabadiliko kama haya.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

118. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN Said (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendeleza Elimu na kufanya majaribio ya mitihani ili kuwapima wanafunzi uwezo wao kielimu, lakini kumekuwa na changamoto ya watoto wa darasa la sita (6) na la saba (7) na la kumi (10) wanakuwa na umri mdogo na kuwa hawana tena nafasi ya kuendelea wala hakuna muongozo wowote wa watoto wale.

(a) Je, ni wanafunzi wangapi wanaotoka darasa la sita, la saba na la kumi kila mwaka.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawekea muongozo wanafunzi ambao hurudia mitihani.

(c) Huu mfumo wa elimu wa kuwatoa watoto darasa la 6, 7, 10 ambao bado ni wadogo na mawazo yao ni ya kitoto na una manufaa gani kwa vijana wetu

Wizara ya Biashara na Viwanda:

199. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Hivi karibuni kumejitokeza baadhi ya wafanyabiashara nchini, kuingiza vyakula visivyo na viwango kwa ajili ya matumzi ya binaadamu na kuhatarisha maisha ya wananchi wetu. Kwa kuwa tatizo hili linaendelea kuwepo.

Je, Wizara inachukuwa hatua gani za kisheria kwa wafanyabiashara hao.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

18. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kumekuwa na malalamiko ya wananchi wa Uroa hasa wakulima ambao wamepata hasara kubwa ya kuvamiwa mazao yao na Kima punju na kupelekea mavuno kidogo. Kwa kuwa Kima punju ni viumbe wanaohifadhiwa kwa shughuli za kuvutia watalii.

Je, kwanini wakulima walioharibiwa mazao yao na Kima punju hawalipwi fedha kama wale wenzao wa Jozani na Pete.

69. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Wananchi wa Maungani, Kisakasaka kwa kipindi kirefu wamechoka kufanyiwa vitendo vya wizi wa mifugo.

(a) Hatua gani zinachukuliwa kukabiliana na wimbi la wizi wa mifugo.

(b) Mifugo mingapi iliyoibiwa imekamatwa pamoja na wahusika wa wizi huo.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2018/2019

Zanzibar,
31 Mei, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.